

“Ni vizuri kuwa na pesa na vitu ambavyo pesa zinaweza kununua, lakini ni vizuri zaidi kuhakikisha hupotezi vitu ambavyo pesa haziwezi kununua.” Hivi ndivyo alivyoandika mwandishi George Horace Lorimer kwenye kitabu chake kinachoitwa Letters from a Self-Made Merchant to His Son.

Kitabu hicho kimesheheni barua za aliyekuwa mfanyabiashara tajiri John Graham kwa kijana wake aliyetitwa Pierrepont akimpa wasia mbalimbali kuhusu maisha, biashara na pesa.

Tunaweza kusema Pierrepont alipata bahati kuwa na baba tajiri, ambaye hakumrithisha tu utajiri, bali alimpa pia ushauri mzuri kuhusu maisha, ikiwepo kujua vitu ambavyo pesa haziwezi kununua, ili kuhakikisha mtu havipotezi kwenye maisha.

Wengi wetu hatujapata bahati ya kuzaliwa kwenye familia zenye utajiri mkubwa na kwa wale wachache waliopata nafasi hiyo, wazazi wao hawakupata nafasi ya kuwapa ushauri muhimu kuhusu pesa kama ambao Graham ametoa kwa kijana wake. Hivyo inapokuja kwenye swala la kutafuta pesa na mali, wengi tunafanya bila ya kuwa na mwongozo sahihi.

Kwenye jamii zetu, hakuna popote tunapofundishwa kuhusu fedha. Kama nilivyoeleza kwa kina kwenye kitabu nilichoandika kinachoitwa ELIMU YA MSINGI YA FEDHA, tangu tunaanza shule mpaka tunahitimu tunaimbiwa wimbo mmoja, soma kwa bidii, faulu vizuri utapata kazi nzuri itakayokupa pesa na mali. Hakuna kingine chochote tunachofundishwa kuhusu pesa.

Tukafundishwa mambo magumu kama historia za miaka mingi iliyopita, miamba mbalimbali ya dunia na hata kanuni mbalimbali za kisayansi, tukakariri kwa juhudi kubwa kwa sababu tulitaka kufaulu mtihani. Lakini kitu kimoja, ambacho tunahangaika nacho maisha yetu yote, hakuna aliyechukua hatua ya kutufundisha.

Na hatuwezi kuwalaumu wazazi au walimu wetu, kwa sababu nao hawakufundishwa, inapokuja swala la pesa na mali, wamekuwa wakiiga kile kinachofanywa na wengine. Haishangazi kwa nini changamoto nyingi kwenye maisha yetu zinahusu fedha.

Mwandishi mashuhuri kwenye eneo la fedha, Robert Kiyosaki amewahi kusema kuna matatizo makuu mawili inapokuja kwenye pesa, kutokuwa na pesa na kuwa na pesa kupitiliza. Hii inaweza kukushangaza kidogo, kwamba

ukiwa huna pesa ni tatizo, ukiwa nazo kupitiliza pia ni tatizo. Hiyo yote ni kwa sababu kuna mambo mengi hatujafundishwa kuhusu pesa.

Tulichoambiwa ni pesa ni kila kitu, tafuta pesa na maisha yako yatakuwa mazuri. Wakati huna pesa maisha yako yanakuwa siyo mazuri, unapambana upate pesa. Na hata unapozipata bado maisha yako yanakuwa siyo mazuri.

Tatizo liko wapi hapa? Kwa nini pesa ziwe mtego mkali hivi, tusipokuwa nazo shida, tukiwa nazo pia shida?

Tunayo bahati kwamba Lackson Tungaraza ametutegulia kitendawili hiki kikubwa kuhusu utafutaji wa pesa na mali. Kwenye kitabu chake hiki kinachoitwa **FUMBO LA PESA NA MALI ZENYE FURAHA**; SIRI zinazowafanya baadhi ya Watu kufurahia Pesa na Mali, huku wengine wakilia na kujuta, Lackson ameweka wazi tatizo liko wapi.

Kwa kutumia historia za maisha ya watu mbalimbali, kuanzia wafalme na manabii waliopita mpaka watu mashuhuri wa zama zetu, Lackson ametuonesha kwa mifano iliyo wazi ni wapi tunapokwama inapokuja kwenye utafutaji wa pesa na mali.

Kuna mengi yamejificha nyuma ya hilo, ambayo hatuyaoni kwa sababu wengi wanaotuzunguka pia hawayaoni. Lakini sasa hatuna tena sababu ya kusema hatukujua, kwa sababu Lackson amepata maono ya kulifunua hili kwa kila mmoja wetu.

Nikusihi usome kitabu hiki kwa kina, ujifunze mambo ya msingi yaliyojificha nyuma ya utafutaji wa pesa na mali, kisha uyaweke kwenye maisha yako. Kwa kuijua misingi hii, utaweza kuondoka kwenye mtego wa pesa, utakuwa tulivu iwe una pesa au huna pesa, kwa sababu unaijua misingi sahihi.

Moja wa watu ambao Lackson amewatumia kutufunulia SIRI zinazowafanya baadhi ya Watu kufurahia Pesa na Mali, huku wengine wakilia na kujuta ni Mfalme Sulemani, mtu tajiri kuliko wote kuwahi kuwepo hapa duniani. Sulemani aliweza kufikia ngazi hiyo ya juu kabisa ya utajiri, siyo kwa kuhangaika na pesa kama wengi wanavyofanya, bali kwa kuzijua SIRI zinazowafanya baadhi ya Watu kufurahia Pesa na Mali, huku wengine wakilia na kujuta

Je na wewe ungependa kuzijua siri hizo?

Usiwe na shaka, zipo ndani ya kitabu hiki cha **FUMBO LA PESA NA MALI ZENYE FURAHA.**

Kisome sasa, elewa misingi sahihi na nenda kaiishi, hutasumbuka tena katika safari yako ya maisha.

Nikutakie kila la kheri katika safari hii ya kuwa na maisha bora yanayojengwa kwenye msingi sahihi.

Kocha Dr Makirita Amani,

www.amkamtanzania.com